# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*

*2015/16*

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2016**

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*
***2015/16***

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

Februari 2016

## Utangulizi

Taarifa hii ya mapitio ya Tamko la Sera ya Fedha inatathmini mwenendo wa utekelezaji wa Sera ya Fedha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2015/16 na kuainisha mwelekeo wa kisera ambao Benki Kuu inakusudia kuchukua katika kipindi kilichobakia cha mwaka wa fedha 2015/16.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2016, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2015, ukilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2014. Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea kiuchumi (*advanced economies*) umeendelea kuimarika, wakati ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua (*emerging market and developing economies*) ukiendelea kukua kwa kasi ndogo. Ukuaji wa uchumi wa mataifa yaliyoendelea uliongezeka na kufikia asilimia 1.9 mwaka 2015, kutoka asilimia 1.8 mwaka 2014 kutokana na kupungua kwa bei za nishati, kuimarika kwa soko la nyumba, na kuwepo kwa ukwasi unaowiana na mahitaji ya uchumi kufuatia muendelezo wa sera ya kuongeza ukwasi katika mataifa hayo (*accommodative monetary policy*). Wakati huo huo, uchumi wa mataifa yanayoibukia kiuchumi na yale yanayoendelea ulikua kwa wastani wa asilimia 4.0, ukilinganishwa na asilimia 4.6, kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa na hali ngumu ya kifedha duniani (*tight global financial conditions*).

Uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2016 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2015. Ukuaji

wa uchumi katika nchi zilizoendelea unatarajiwa kuendelea kuimarika ukichangiwa na mwenendo mzuri katika sekta ya fedha, kuimarika kwa masoko ya nyumba na ajira, kushuka kwa bei za nishati pamoja na kuongezeka kwa kipato. Ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea unatarajiwa kuongezeka hasa katika nchi ya India. Hata hivyo, ukuaji wa uchumi wa China unatarajiwa kupungua kutokana na kushuka kwa kasi ya uwekezaji. Ukuaji uchumi wa nchi za Afrika zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara unatarajiwa kuimarika, ingawa ukuaji huo unategemewa kuathiriwa kwa kiasi na kushuka kwa bei za bidhaa pamoja na gharama kubwa za ukopaji.

Mfumuko wa bei kwa baadhi ya nchi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi uliongezeka mwishoni mwa mwaka 2015, baada ya kipindi kirefu cha viwango vidogo vya mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei uliongezeka nchini Marekani, Uingereza, China na nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya; wakati nchini India mfumuko wa bei umeendelea kubaki chini ya sifuri (*deflation)* kwa kipindi cha miezi kumi na tatu mfululizo, kutokana na kushuka kwa bei za madini, mafuta na nishati, vinywaji, tumbaku, mbao na karatasi. Mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 7.1 mwezi Desemba 2015, wakati ule wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ulifikia asilimia 7.4 kutokana hasa na uhaba wa chakula.

Kwa mujibu wa taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Januari 2016, mfumuko wa bei unatarajiwa kuongezeka hadi wastani wa asilimia 1.1 mwaka 2016, kutoka asilimia 0.3 mwaka 2015 katika nchi zilizoendelea. Katika nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea, mfumuko wa bei unatarajiwa

kuongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2016 kutoka asilimia 5.5 mwaka 2015, hususan kutokana na madhara ya kushuka kwa thamani ya sarafu katika nchi hizo.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### Tanzania Bara

Katika kipindi cha robo tatu za mwanzo za mwaka 2015, uchumi umeendelea kuimarika na kukua kwa wastani wa asilimia 6.9 ukilinganishwa na matarajio ya ukuaji wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2015. Kiwango hiki cha ukuaji wa uchumi kimechangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya miundombinu pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji kwenye utoaji wa huduma za simu na intaneti. Hali hii pia ilichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya uzalishaji umeme kulikopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani na huduma nyingine; pamoja na kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na kuimarika kwa uchumi wa dunia.

Mfumuko wa bei uliongezeka kidogo katika nusu ya pili ya mwaka 2015 kutokana hasa na kupanda kwa bei za vyakula. Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 6.8 katika mwaka ulioishia mwezi Desemba 2015, ukilinganishwa na asilimia 6.1 kwa mwezi Juni 2015. Wakati huo huo, mfumuko wa bei usiojumuisha chakula na nishati (*core inflation*) uliendelea kubaki katika viwango vya chini ya asilimia 2.5 kutokana na hatua mbalimbali za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2015/16, takwimu za mapato yaliyokusanywa na kuhifadhiwa kwenye akaunti za serikali Benki Kuu ya Tanzania yalikuwa shilingi bilioni 6,608.3 sawa na asilimia 98.1 ya makadirio, kiasi ambacho kilikidhi gharama za matumizi ya kawaida ya serikali katika kipindi hicho. Kiasi hicho pia kilikuwa asilimia 29.3 juu zaidi ya kiwango kilichokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/15. Mafanikio makubwa yameonekana katika makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwezi Novemba na Desemba 2015, ambapo makusanyo yalivuka malengo kwa asilimia 3.6 na 6.2, kwa matiririko huo. Matumizi ya serikali yalikuwa shilingi bilioni 8,423.6 sawa na asilimia 92.1 ya makadirio, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 6,607.2.

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2015, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*) ulipungua kwa asilimia 44.2 na kufikia dola za Kimarekani milioni 1,161.9 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani milioni 2,081.1 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Kupungua huko kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje kulitokana na ongezeko la thamani ya mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani na mapato yatokanayo na utalii na huduma za usafirishaji, pamoja na kupungua kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje hususan uagizaji wa mafuta, vifaa vya ujenzi na chakula. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Kimarekani milioni 4,093.7 mwishoni mwa mwezi Desemba 2015, ambazo zinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4. Aidha, rasilimali za fedha za kigeni za mabenki ya biashara zilifikia dola za Kimarekani milioni 1,012.1, wakati amana za fedha za kigeni za sekta binafsi katika mabenki zilifikia dola za Kimarekani milioni 2,933.1 mwishoni mwa mwezi Desemba 2015.

Deni la nje liliongezeka kwa asilimia 0.1 hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 15,408.5 mwishoni mwa mwezi Desemba 2015, likilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 15,395.7 mwishoni mwa mwezi Juni 2015. Kati ya deni hilo, asilimia 84.8 ilikuwa ni deni la serikali na taasisi za umma. Tathmini ya hivi karibuni ya uhimilivu wa deni la nje inaonesha kwamba thamani halisi ya deni la nje ikilinganisha na pato halisi la Taifa ilifikia asilimia 20.0 mwishoni mwa mwezi Juni 2015, ambayo ni chini ya ukomo uliowekwa kimataifa wa asilimia wa 50.0. Hii inamaanisha kwamba deni la nje la Tanzania bado ni himilivu. Deni la ndani liliongezeka kwa asilimia 13.2 hadi shilingi bilioni 8,597.0 mwishoni mwa mwezi Desemba 2015 kutoka shilingi bilioni 7,594.7 mwishoni mwa mwezi Juni 2015. Ongezeko hilo lilitokana na uuzaji wa dhamana za Serikali kwa ajili ya kugharamia bajeti ya serikali.

Sekta ya kibenki imeendelea kukua ikichangiwa pamoja na mambo mengine na uanzishwaji wa taasisi mpya za kifedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Takwimu za awali za tathmini ya hali ya mabenki yetu zinaonesha kuwa mabenki hayo ni imara na salama, yakiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha, na pia mikopo chechefu imeendelea kupungua.

Hali ya mfumo wa malipo nchini imeendelea kuimarika chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania, na matumizi yake yameendelea kuongezeka kwa kasi. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuendelea kukua kwa imani ya matumizi ya teknolojia na intaneti, ambapo matumizi ya simu za mkononi kama njia ya kupata huduma za kifedha yamekua kwa kasi na hivyo kuipatia Tanzania sifa ya kuwa na ubunifu katika utoaji huduma za kifedha kimataifa. Hadi mwishoni mwa mwezi Desemba 2015, idadi ya

watumiaji hai wa huduma za kifedha kwa njia ya simu za mkononi (active users) ilikuwa milioni 19.0. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania imechapisha kanuni za uendeshaji wa mifumo ya malipo (Licensing and Approval regulations, 2015 na Electronic Money Issuance regulations, 2015) ikiwa ni mkakati wa utekelezaji na usimamizi wa Sheria ya Mifumo ya Malipo Nchini ya mwaka 2015 (National Payment Systems Act, 2015).

Benki Kuu ya Tanzania imeimarisha usimamizi na udhibiti wa taasisi za fedha kwa kupitia na kutoa muongozo mpya wa namna ya uwekezaji rasilimali katika mifuko ya hifadhi ya jamii (*Social Security Investment Guidelines*, *2015*); kutoa upya kanuni za mabenki na taasisi za kifedha kuhusu mikopo ya nyumba (*Banking and Financial Institutions - Mortgage Finance -Regulations, 2015*); na kanuni za maduka ya fedha za kigeni (*Bureau de Change Regulations, 2015*). Marekebisho haya yalifanywa ili kuhusisha maendeleo ya hivi karibuni katika masoko ya fedha; na pia kuwezesha Benki Kuu kutekeleza kwa ufanisi zaidi jukumu lake la kusimamia masuala yote yanayohusu sekta ya fedha.

**Zanzibar**

Katika kipindi cha robo tatu za mwanzo za mwaka 2015, Pato la Taifa la Zanzibar lilikua kwa asilimia 4.6 likilinganishwa na asilimia 9.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi, ulichangiwa na ukuaji katika sekta ya viwanda, fedha na bima, uvuvi na shughuli za utalii hususan huduma za malazi na chakula. Mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 11.7 kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2015 ukilinganishwa na asilimia 3.9 mwezi Juni 2015. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa baadhi ya bei za vyakula hasa samaki, mchele, ngano na sukari.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2015/16, mapato ya ndani ya serikali yalifikia shilingi bilioni 189.8, kiasi ambacho kilikidhi gharama za matumizi ya kawaida kwa kipindi hicho. Mapato yote yalikuwa sawa na asilimia 89.3 ya makadirio wakati mapato yatokanayo na kodi yalikuwa shilingi bilioni 174.6, sawa na asilimia 89.0 ya makadirio. Misaada ilifikia kiasi cha shilingi bilioni 14.5 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi bilioni 2.9. Jumla ya matumizi ilikuwa shilingi bilioni 218.8, kati ya hizo matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 183.4.

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2015, ziada katika urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ilifikia dola za Kimarekani milioni 12.2, ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 18.8 iliyorekodiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2014. Hali hii ilichangiwa na kupungua kwa mauzo ya karafuu nchi za nje, pamoja na kupungua kwa fedha za kigeni kutoka kwa washirika wa maendeleo, ambazo hazikuweza kufidiwa kwa kupungua kwa thamani ya uagizaji mafuta kwa takriban asilimia 20.5, kulikotokana na kushuka kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia.

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2015/16

### *Malengo ya Sera ya Fedha*

Ili kufikia malengo ya serikali ya uchumi jumla, Benki Kuu imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kutimiza malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslimu usiozidi asilimia 13.4;
ii. Ukuaji wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 16.0;
iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 19.3; na

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

***Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2015/16***

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2015/16, hali ya ukwasi kwa ujumla katika mabenki ilikuwa ya kuridhisha licha ya kuwepo kwa vipindi vichache vya upungufu. Hali ya upungufu wa ukwasi ilijitokeza zaidi mwanzoni mwa mwaka wa fedha kufuatia matumizi madogo ya serikali, pamoja na matokeo ya hatua mbalimbali za sera ya fedha zilizochukuliwa na Benki Kuu katika robo ya mwisho ya mwaka 2014/15 ili kudhibiti matarajio ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei na athari za kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Kutokana na hali hii, riba katika soko la fedha baina ya mabenki iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 29.98 mwezi Julai 2015 kutoka asilimia 17.99 mwezi Juni 2015.

Hali ya ukwasi ilianza kuimarika mwezi Agosti 2015, kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya serikali. Viwango vya riba katika soko la fedha baina ya mabenki vilipungua na baadaye kupanda tena kuanzia mwezi Oktoba 2015, kufuatia kuongezeka kwa fedha zilizoko nje ya mabenki kulikochangiwa zaidi na shughuli za uchaguzi mkuu. Fedha zilizoko nje ya mabenki ziliongezeka zaidi katika miezi ya Novemba na Desemba 2015 kutokana na ongezeko la mahitaji ya msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka. Hata hivyo, viwango vya riba katika soko la fedha viliendelea kuwa vya wastani kwani mabenki yalikuwa na ukwasi wa kutosha uliotokana na serikali kufanya malipo makubwa katika kipindi

hicho. Aidha, hali ya ukwasi kwa baadhi ya mabenki ilipungua katika wiki ya mwisho ya mwezi Desemba 2015 kufuatia msimu wa malipo ya kodi ya mapato. Katika kukabiliana na hali ya upungufu wa ukwasi, baadhi ya mabenki yalikopa Benki Kuu kupitia madirisha yake ya ukwasi.

Ukuaji wa ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi ulibaki ndani ya malengo. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 18.0 kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2015, sawa na makadirio katika kipindi hicho, wakati mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 24.8, ikilinganishwa na makadirio ya asilimia 24.0.

Thamani ya shilingi iliyoporomoka katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2014/15 ilianza kuimarika mwezi Agosti 2015 kufuatia matokeo ya hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania. Kuporomoka kwa thamani ya shilingi katika robo ya mwisho ya mwaka 2014/15 kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuimarika kwa dola ya Kimarekani, kulikoambatana na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za kigeni kwa ajili ya bajeti ya serikali pamoja na mapato madogo ya fedha za kigeni yatokanayo na mauzo ya mazao ya biashara, na hivyo kusababisha kuongezeka kwa biashara ya maoteo kwenye ubadilishaji wa shilingi na dola ya Marekani (speculative tendencies).

### *Matarajio ya Uchumi*

Uchumi unatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi ya juu ukichangiwa zaidi na uwekezaji katika miundombinu; kuongezeka kwa shughuli za ujenzi katika sekta binafsi na ya umma; ukuaji katika sekta ya viwanda kutokana na upatikanaji wa umeme wa uhakika unaochangiwa na kuendelea kuongezeka kwa vyanzo vya uzalishaji umeme; kushuka kwa bei ya

mafuta duniani; ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi; pamoja na kuimarika kwa uchumi wa nchi zilizoendelea. Pamoja na hayo, uboreshaji wa utoaji wa huduma za kifedha, hasa huduma za malipo kupitia simu za mkononi utaendelea kusaidia ukuaji wa shughuli za uchumi mpana.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa wa wastani na kubakia katika tarakimu moja katika miezi ijayo, kufuatia upatikanaji mzuri wa chakula unaotokana na mvua za vuli, pamoja na bei ndogo ya mafuta nchini inayotokana na kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na kupungua kwa kasi ya kushuka kwa thamani ya shilingi. Pia, kuendelea kutekeleza sera madhubuti ya fedha na usimamizi mzuri wa matumizi na mapato ya serikali kutasaidia kupunguza kasi ya mfumuko wa bei. Aidha, ipo hatari ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei kutokana na upungufu wa mavuno ya mazao ya chakula uliojitokeza kwa baadhi ya nchi jirani.

Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali na nchi za nje unatarajiwa kuimarika zaidi ukichangiwa na ongezeko la thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi pamoja na mapato yatokanayo na utalii, pamoja na kushuka kwa thamani ya uagizaji wa mafuta kufuatia kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia. Sambamba na hali hiyo, inatarajiwa kwamba thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani itabaki tulivu zaidi katika miezi ijayo.

Sekta ya kibenki inatarajiwa kuendelea kuimarika kukichangiwa zaidi na jitihada zinazoendelezwa na Benki Kuu ya Tanzania za kuboresha usimamizi wa taasisi za fedha nchini. Pia, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuboresha mfumo wa malipo nchini ambao ni salama ili kudumisha utulivu wa sekta ya fedha nchini na kuboresha masoko ya fedha kwa manufaa ya uchumi kwa ujumla.

***Mwenendo wa Sera ya Fedha katika Nusu ya Pili ya 2015/16***

Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera madhubuti ya fedha kwa kutumia zana mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha kwamba mahitaji ya ukwasi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi yanafikiwa bila ya kuchochea mfumuko wa bei. Katika juhudi za kuongeza ufanisi wa soko na utulivu wa viwango vya riba katika soko la fedha, Benki Kuu itaimarisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali muhimu za kimasoko kati yake na mabenki ya biashara ili yaweze kusimamia kwa makini mahitaji yake ya ukwasi. Wakati huo huo, Benki Kuu ipo katika hatua za awali za maandalizi ya kutumia riba za muda mfupi (*short-term interest rate*) kama nyenzo kuu ya kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha, sambamba na juhudi za kuoanisha (*harmonization*) sera za fedha baina ya nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

**Hitimisho**

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2015/16, Benki Kuu ilitekeleza sera madhubuti ya fedha ili kudhibiti kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei kutokana na kupanda kwa bei za vyakula na kasi ya kushuka kwa thamani ya shilingi. Katika kipindi hicho, ukuaji wa ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi ulibakia ndani ya malengo.

Ukuaji wa uchumi umeendelea kuimarika  na mfumuko wa bei ukibaki ndani ya kiwango cha tarakimu moja. Uchumi unatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi nzuri, ukichangiwa zaidi na uwekezaji katika miundombinu, kuendelea kukua kwa shughuli za ujenzi katika sekta binafsi na ya umma, ukuaji katika sekta ya viwanda, kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, pamoja na matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa dunia. Mfumuko

wa bei unatarajiwa kubaki katika viwango vya tarakimu moja hasa kutokana na kushuka kwa bei ya nishati, utulivu katika kasi ya kushuka kwa thamani ya shilingi, pamoja na sera madhubuti ya fedha na usimamizi thabiti wa matumizi na mapato ya serikali. Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali na nchi za nje unatarajiwa kuimarika zaidi kutokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii, mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi, mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji, pamoja na kushuka kwa bei ya mafuta duniani.

Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuchukua tahadhari dhidi ya athari za upungufu wa mavuno ya mazao ya chakula kwa baadhi ya nchi jirani, ili kudhibiti hatari ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei. Kwa kuzingatia hili, Benki Kuu imejizatiti na ipo tayari kuchukua hatua za ziada za kisera ili kuhakikisha kwamba mfumuko wa bei unaendelea kuwa tulivu.

Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuboresha utendaji wa soko la fedha kwa kuimarisha mawasiliano baina yake na wadau wa soko la fedha, pamoja na kuimarisha usimamizi katika sekta ya mabenki. Wakati huo huo, juhudi zinafanyika ili kuboresha mfumo wa sera ya fedha unaotarajiwa kuwezesha Benki Kuu ya Tanzania kufikia malengo yake kirahisi. Kutokana na matokeo mazuri ya utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2015/16, ni matarajio ya Benki Kuu kuwa malengo ya Sera ya Fedha kwa mwaka 2015/16 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz

Kimepigwa Chapa na Identity Promotion Ltd